

3

١٠

KOHELETH.

SO
LI
DEO
GL
OR
IA

ZANZIBAR:
PRINTED AT THE UNIVERSITIES' MISSION PRESS
1888.

KOHELETH ; ao MHUBIRI.

SURA 1.

- M**ANENO ya Mhubiri, mwana wa Daud, Mfalme katika Yerusalemi.
- 2 Ubatili wa ubatili, asema Mhubiri; uba-
3 tili wa ubatili, vyote ubatili. Yamfaa
nini mwana wa Adamú matendo yake yote,
4 ayatendayo chini ya jua? Kizazi chaenda,
kizazi chaingia; nayo dunia yasimama da-
5 yima. Jua tena laondoka, jua lashuka, la-
6 fanya haraka kwake, laondokako. Upepo
ukienda kusini, ukigeuka kaskazini, kuge-
uka ukigeuka, waenda; na kwa kugeuka
7 kwake warudi upepo. Mito yote huendea
bahari, wala bahari haijawi; kuko huko
8 mito iendako, ndiko irudiko. Yote yenyi
kuchosha; hawezi mtu kunena: halishibi
jicho kwa kuona, wala sikio halijawi kusi-
9 kia. Lililokuwa lile litakalokuwa; nalo
lililofanyika lile litakalofanyika: wala ha-
10 pana lililo jipya chini ya jua. Liko neno
liambiwalo, Tazama, jipya hili? limekwi-
sha kuwa zamani zilizokuwako kabla yetu.
11 Vilivyo kwanza havina kumbukumbu; wa-
la havitakuwa na kumbukumbu vya mwi-
sho vitakavyokuwa kati mwao watakao-
kuwa baadaye.

- 12 Mimi mhubiri nilikuwa mfalme juu ya
 13 Israeli katika Yerusalemi. Nikatia moyo
 nitafute nikapeleleze kwa hekima yote ya-
 fanywayo chini ya mbingu: utumwa mba-
 ya huu Muungu aliowapa waana Adamu,
 14 wautumikie. Nimeona matendo yote ya-
 liyotendeka chini ya jua; na, taza **g**a, yote
 15 ubatili, na kupapia upepo. Yaliyopotoka
 hayanyosheki: nayo ihtilafu hayahesabiki.
 16 Naliwaza moyoni mwangu mimi, nikasema,
 Mimi, tazama, nimejiongezea hekima na
 kuzidi kuliko wote waliokuwako Yerusale-
 mi mbele yangu: na moyo wangu umeona
 17 wingi wa hekima na maarifa. Nalitua
 moyo nijue hekima, nikajue upumbafu na
 ujinga; nikatambua haya pia ni kupapia
 18 upepo. Kwani kwa wingi wa hekima wi-
 ngi wa huzuni: naye aongezaye maarifa
 huongeza sikitiko.

SURA 2..

- N**ALISEMA mimi moyoni mwangu,
 Haya bassi, nitakujaribu kwa furaha;
 bassi ujifurahishe na mema: na, tazama,
 2 haya tena ubatili. Nikakinenea kicheko,
 3 Ni upumbafu: na furaha, Yafanyaje? Na-
 lipeleleza moyoni mwangu, nipateje kuji-
 burudisha mwili na mvinyo, moyo wangu
 bado ukiongoza kwa hekima, na ginsi ni-
 ushike upumbafu, hatta nitakapona yaliyo
 mema kwa waana Adamu wayatende chi-
 ni ya mbingu hesabu ya siku za maisha yao.

- 4 Kazi zangu nikazifanyiza kubwa; nikajije-
 5 ngea nyumba; nikajipandia mizabibu; ni-
 kajifanyizia bustani na mashamba, nikaya-
 pandia miti ya namna zote za matunda;
 6 nikajifanyizia mabirika ya maji, niunyesheshe
 7 nayo mwitu ilimopandwa miti: nikanunua
 watwana na wajakazi, wakazaliwa watumi-
 shi nyumbani kwangu; tena nikawa na mali
 nyingi za ng'ombe na kondoo kupita wote
 8 walioko Yerusalemi mbele yangu: nikaji-
 kusanyia tena fetha na thahaba, na t'umu
 za wafalme na za inchi: nikajipatia wa-
 imbaji waume na waimbaji waanake, nazo
 banassa za waana Adamu, masuria wengi
 9 sana. Bassi nikawa mkubwa, nikaongezeka
 kuliko wote waliokuwako Yerusalemi
 10 mbele yangu: tena hekima yangu ikanisi-
 mamia. Wala sikuzuia macho yangu ka-
 tika killa kilichotamanika nayo: wala si-
 kunyima moyo wangu furaha yo yote, kwa-
 ni moyo wangu uweifurahia kazi yangu
 yote; yakawa haya sehemu yangu katika
 11 kazi yangu yote. Nikaangalia mimi ma-
 tendo yote mikono yangu iliyoyatenda, na
 kazi yote niliyosumbua kufanyiza: na, ta-
 zama, yote ubatili na kupapia upepo, wala
 chini ya jua hapana kufaa.
 12 Nikaangalia nitazame hekima, na upu-
 mbafu na ujinga: kwani *aweza* nini mwa-
 na Adamu atakayekuja baada ya mfalme?
 13 yale yaliyokwisha kufanyizwa. Nikaona
 mimi hekima kuwa bora kuliko upumbafu,
 14 kama nuru bora kuliko giza. Mwenyi

- hekima macho yake kitwani mwake, naye mpumbafu hueuda gizani: nikaona mimi
 15 lakini tukio moja liwapatalo wote. Nika-
 sema mimi moyoni, Limpataavyo mpumbafu
 ndivyo litakavyonipata mimi; nami bassi
 mbona nalikuwa na hekima zayidi? Ni-
 kasema moyoni, kama haya pia ubatili.
 16 Kwani hana kumbukumbu la milele mwenyi
 hekima kama mpumbafu; wakiwa siku zi-
 takazokuja wote watakuwa wamekwisha
 kusahauliwa. Na ginsi mwenyi hekima a-
 farikivyo kama mpumbafu vile! Bassi
 nikauchukia uhayi; kwa kuwa mbaya
 kwangu kazi iliyotendeka chini ya jua:
 kwani yote ubatili na kupapia upepo.
 17 Nikachukia mimi shughuli yangu yote
 18 niliyoshughulika chini ya jua: nikiwa sina
 buddi nimwachie mwana Adamu atakaye-
 19 kuwa baada yangu. Na nani ajuaye kama
 atakuwa mwenyi hekima, ao mpumbafu?
 naye ataimiliki shughuli yangu yote uiliyo-
 ishughulikia, niliyoionyeshea hekima chini
 20 ya jua. Haya tena ubatili. Kwa hiyo ni-
 katangatanga kujitilia moyo mashaka ya
 shughuli yote niliyoshughulikia chini ya
 21 jua. Kwani yuko mwana Adamu ashughu-
 likaye kwa hekima, na kwa maarifa, na kwa
 ustadi; nayo ataitoa kuwa sehemu yake
 mwana Adamu asiyeshughulika nayo. Ha-
 22 ya pia ubatili na ubaya mkuu. Kwani
 nini aliyo nayo mwana Adamu kwa shu-
 ghuli yake yote, na kwa kusumbuka moyo,
 23 aliyoshughulikia chini ya jua? Kwani

siku zake zote masikitiko na utumwa wake huzuni; hatta usiku pia moyo wake humpumziki. Haya tena ubatili.

- 24 Hana lililo jema mwana Adamu kuliko kula na kunywa na kujifurahisha roho na mema kwa shughuli yake. Haya teno nimeyaona mimi yatokayo mkononi kwa
- 25 Muungu. Kwani nani awezaye kula, na nani awezaye kufurahiwa kuliko mimi?
- 26 Kwani humpa hekima na maarifa na furaha mwana Adamu ampendezaye; naye humpa mwenyi thambi utumwa, azoe akakusanyo ya kumpa yeye ampendezaye Muungu. Haya tena ubatili na kupapia upepo.

SURA 3.

- K**ILLA kitu na muhulla wake, hatta killa jambo chini ya mbingu na wakati wake : wakati wa kuzaliwa, na wakati wa kufa; wakati wa kupanda, na wakati wa kung'oa yaliyopandwa; wakati wa kua, na wakati wa kuponya; wakati wa kubomoa, na wakati wa kujenga; wakati wa kulia, na wakati wa kucheka; wakati wa kuomboleza, na wakati wa kucheza; wakati wa kutupa mawe, na wakati wa kukusanya mawe; wakati wa kushikamena, na wakati wa kufarakana; wakati wa kutafuta, na wakati wa kupoteza; wakati wa kutunza, na wakati wa kutupa; wakati wa kurarua, na wakati wa kushona; wakati wa kunyamaza, na wakati wa

6 KOHELETH ao MHUBIRI, 3.

8 kusema; wakati wa kupenda, na wakati
wa kuchukia; wakati wa vita, na wakati
9 wa amani. Yamfaa nini atendaye yale
10 anayoyashughulikia? Nimeuona utumwa
Muungu aliowapa waana wa Adamu wau-
11 tumikie. Amefanyizia uzuri killa kitu
wakati wake: tena amewawekea ulimwengu
moyoni, yasitafutikane lakini na mwana
Adamu matendo aliyoyatenda Muungu
12 tangu mwanzo hatta mwisho. Najua
hapana lililo jema kwao kuliko kufurahiwa
13 na kutenda mema kadiri waishivyo. Tena
apate killa mwana Adamu kula na kunywa
na kufurahiwa nayo mema kwa shughuli
14 yake yote, karamu ya Muungu hii. Najua
yote, ayafanyayo Muungu, yatakuwa ya
milele haya: hayawezekani kuzidishiwa
kitu, wala kuondolewa kitu: na Muungu
15 aliyoyafanya, waone hofu mbele yake. Lile
lililoko limekuwa zamani, na lile litakalo-
kuwa limekuwa zamani: naye Muungu
hutafula tena yaliyofukuzwa.
16 Hatta tena nikaona chini ya jua mahali
pa hukumu uko uovu; na mahali pa haki
17 uko uovu. Nikasema mimi moyoni, Muungu
atawahukumu wenyi haki na waovu: kwani
killa jambo na killa kazi huko na wakati
18 wake. Nikasema mimi moyoni, Mambo
ya waana Adamu, Muungu awathubutishe,
nao wajione kwa nafsi zao kuwa nyama.
19 Kwani tukio lao waana Adamu tukio lao
nyama; nalo moja liwatukialo: kama
afarikivyo huyu afariki na huyu: hatta

- pumuzi moja wanayo wote: wala mwana Adamu hawapiti nyama: kwani yote ubatili.
- 20 Wote huenda palepale; wametoka mavumbini wote, na mavumbini hurudi wote.
- 21 Nani ajuaye roho ya waana Adamu, kama inapanda hii juu, na roho ya nyama, kama
- 22 inashuka hii chini hatta inchi? Nikaona kama hapana lililo jema, kuliko mwana Adamu azifarahie kazi zake: kwani sehemu yake hii; kwani nani atakayemleta ayaone yatakayokuwa baada yake?

SURA 4.

- N**IKARUDI nikaona mathalimu yote yanayofanyika chini ya jua: na, tazama, machozi yao waliothulumiwa, wala hawana wa kuwafariji; mkononi mwao waliowathulumia uwezo, wala hawana wa kuwafariji.
- 2 Nikawasifu mimi wafu waliokwisha kufa zayidi ya wahayi walio na uhayi
- 3 bado; naye heri kuliko wao wote asiyekuwa bado, asiyeona matendo mabaya yaliyofanyika chini ya jua.
- 4 Nikaona mimi kazi yote na killa tendo la ustadi, ya kuwa uwivu wa mtu kwa jirani yake naye. Haya tena ubatili na
- 5 kupapia upepo. Mpumbafu amekunjana
- 6 mikono, hula mwili wake mwenyewe. Heri ukufi kwa utulivu, kuliko magao mawili kwa kushughulika na kupapia upepo.
- 7 Nikarudi mimi, nikaona ubatili chini ya
- 8 jua. Yuko aliye mmoja, wala wa pili hana;

- hatta mwana wala ndugu hana ; wala shughuli yake yote haina mwisho, wala macho yake hayashibi na utajiri. Nani bassi namfanyizia kazi, namzuilia mema roho yangu? Haya tena ubatili, hatta
- 9 utumwa mbaya huu. Heri wawili kuliko mmoja ; kwani wanayo ijara njema ya kazi
- 10 yao. Kwani wakianguka, mmoja atamwina mwenzake : lakini ole wake aliye wa pekee aangukapo, wala hana mwingine wa
- 11 kumwinulia. Tena wawili wakilala pamoja, ndipo watakuwa na moto : lakini mmoja
- 12 awezaje kuwa na moto? Hatta yule wa pekee akishindwa na mtu, wawili watampinga ; wala kamba ya meno matatu haikatiki upesi.
- 13 Heri kijana maskini mwenyi hekima kuliko mfalme mzee mpumbafu, asiyejua
- 14 kurudika tena. Kwani katika nyumba ya kufungwa ametoka kumiliki ; kweli hatta kwa kumiliki kwake amezaliwa maskini.
- 15 Naliwaona wahayi wote watembeao chini ya jua, walikuwa naye kijana, yule wa pili aliyesimama mahali pake. Hawakuwa na
- 16 mwisho watu wote, hatta wale wote aliokuwa juu yao : wallakini wale wafuatao hawatamfurahia. Hakika haya tena ubatili, na kupapia upepo.

SURA 5.

UJITUNZE mguu wendapo nyumbani kwa Muungu ; kwani heri kukaribia usikie

- kuliko kutoa sadaka ya wapumbafu : kwani
 2 hawajui kwamba wafanya mabaya. Usikose utaratibu kwa kinwa chako, wala moyo wako usiwe mpesi kutoa neno mbele ya Muungu; kwani Muungu mbinguni na wewe katika inchi: kwa hiyo na nawe
 3 maneno yako machache. Kwani huja ndoto kwa wingi wa utumwa; na sauti ya mpumbafu kwa wingi wa maneno. Umwekeapo Muungu nathiri, usikawie kuiondoa; kwani huawafurahii wapumbafu : ondoa
 5 uliloliweka. Afathali usiweke, kuliko
 6 uweke usiondoe. Usiache kinwa chako kukosesha mwili wako; wala usiseme mbele ya malaika, kwamba umepitiwa: kwa nini Muungu akasirike na sauti yako,
 7 aharibu kazi ya mikono yako? Kwani kwa wingi wa ndoto, na ubatili, na maneno mengi, haya : lakini Muungu umwogope wewe.
 8 Ukiona maskini kuonewa, na kuondolewa kwa jeuri hukumu na haki katika ufalme, usilitaajabia jambo, kwani aliye juu kuwapita walio juu aangaliaye, wakiwa walio
 9 juu kuwapita hao. Nayo manofaa ya inchi kwayo yote : mfalme atumikiwa na koondo,
 10 Apendaye fetha hatashiba na fetha; wala apendaye wingi na mazao : haya tena
 11 ubatili. Mema yakiongezeka, waongezeka nao walao : naye mwenyewe afayidiwa nini.
 12 illa kutazama kwa macho tu? Usingizi wake atumikaye mtamu akila kidogo akili

10 KOHELETH ao MHUBIRI, 5.

chingi: lakini kushiba kwake tajiri haku-
mwachi kulala usingizi.

- 13 Kiko kinicho kibaya kizito nilichokiona
chini ya jua, mali zilizoshikwa na mwenye-
14 we kwa hasara yake; na mali hiyo hupotea
kwa utumwa mbaya; naye akiwa amemzaa
mwana, hapana kitu mkononi mwake.
15 Alivyotoka tumboni mwa mamaye, uchi
atarudi kwenda kama alivyokuja, wala
hatachukua kitu cha kazi yake, cha kupe-
16 lekea mkononi. Nayo pia mabaya mazito,
vile alivyokuja, vile atakwenda: na nini
iliyomfaa kuwa ameushughuhkia upepo?
17 Siku zake zote tena hula gizani, akiwa na
uchungu mwingi, mwengi ugonjwa na
hasira.
18 Tazama, niliyoyaona mimi mema na
yaliyo mazuri, kula na kunywa na ku'ura-
hiwa na mema kwa shughuli yake yote,
ashughulikiayo chini ya jua hesabu ya siku
zake, alizompa Muungu: kwani hii sehemu
19 yake. Tena killa mwana Adamu Muungu
aliyempa mali na utajiri, aliyemwezesha
kula nayo, na kuchukua sehemu yake, na
kuifurahia shughuli yake, karamu ya
20 Muungu hii. Kwani hatakumbuka mno
siku za maisha yake, kwa kuwa Muungu
atakabali moyo wake ukifurahia.

SURA 6.

UKO ubaya niliouona chini ya jua, nao
mwingi juu ya waana Adamu:

- 2 mtu aliyepewa na Muungu mali, utajiri; heshima, asihitaji kitu roho yake katika yote atamaniyo, wala Muungu hamwezeshi kula nayo, lakini hula mtu mgeni; haya
- 3 tena ubatili, na ugonjwa mbaya huu. Mtu akizaa mia, akiishi miaka mingi, nayo siku za maisha yake nyingi, ilakini roho yake haikushiba mema, tena akikosa maziko; nasema, Heri nimba iliyoharibika kuliko
- 4 yeye: kwani kwa ubatili huja, na gizani huenda, nalo jina lake hufunikwa kwa giza
- 5 tena jua haikuliona wala kujua; imestarehe
- 6 hii kuliko yule: kweli, ajapoishi miaka elfu marra mbili, wala hafurahiwi na mema: si
- 7 palepale waendapo wote? Shughuli yote ya mwana Adamu kwa kinwa chake, wala
- 8 nafsi yake haikujazwa. Kwani amefayidiwa nini mwenyi bekima kuliko mpumbafu? nini anayo maskini ajuaye kutembea mbele
- 9 yao wahayi? Heri kuona kwa macho kuliko kutembea kwa roho: haya tena ubatili, na kupapia upepo.
- 10 Killa kilichokuwa, kimekwitwa jina lake zamani, kimejulikana kama wa Adamu huyu: wala hawezi kushindana naye aliye
- 11 na nguvu kuliko yeye. Yakiwa maneno mengi yaongezayo ubatili, afayidiwa
- 12 nini mwana Adamu? Kwani nani ajuaye yaliyo mema ya mwana Adamu akiishi, hesabu ya siku zake za ubatili, azitumazo kama kivuli? kwani nani atakayemweleza mwana Adamu yatakayokuwa baada yake chini ya jua?

SURA 7.

HERI sifa kuliko marhamu mazuri; na
 2 siku ya kufa kuliko siku ya kuzali-
 wa. Heri kuiendea nyumba ya matanga,
 kuliko kuiendea nyumba ya karamu: kwani
 mwisho huo wa waana Adamu wote; naye
 3 aliye hayi atatia moyoni. Heri huzuni
 kuliko kicheko: kwani kwa sikitiko la
 4 uso moyo hufanikiwa. Mioyo yao wenyi
 hekima katika nyumba ya matanga: lakini
 mioyo yao wapumbafu katika nyumba ya
 5 furaha. Heri kusikia laumu yao wenyi
 hekima kuliko mtu asikie uimbo wa wa-
 6 pumbafu. Kwani kama makelele ya miiba
 chini ya sufuria, kicheko cha mpumbafu
 7 vile: haya tena ubatili. Kweli jeuri humpu-
 mbazisha mwenyi hekima; na zawadi hua-
 8 ribu akili. Heri mwisho wa neno kuliko
 mwanzo wake: mvumulivu wa roho heri
 9 kuliko mwenyi roho ya juu juu. Usifanye
 haraka rohoni: kwani hasira ikaayo vifuani
 10 mwa wapumbafu. Usiseme, Kuna nini kuwa
 siku za zamani heri kuliko hizi? kwani
 11 si katika hekima uyaulize haya. Hekima
 njema kama milki: hatta bora kwao waonao
 12 jua. Kwani hekima uvuli, kama fetha
 uvuli: na fayida yake maarifa, hekima
 13 humhifathi hayi aliye nayo. Uifikiri kazi
 ya Muungu: kwani nani awezaye kuya-
 14 nyosha yale aliyoyapotosha? Siku ya
 mema ufurahi, siku ya mabaya ufikiri:
 amefanya na hizo Muungu sawa sawa pa-

moja, yasipate kutafutikana na mwana Adamu ya baada yake.

- 15 Haya yote nimeyaona siku za ubatili wangu: yuko mwenyi haki apoteaye kwa haki yake, yuko na mwovu azidishaye
- 16 *maisha* kwa ubaya wake. Usiwe na haki kwa mno: wala usijiongezee hekima sana:
- 17 kwa nini ujiharibu? Usiwe mwovu kwa mno, wala usipumbazike: kwa nini ufe
- 18 kabla ya wakati wako? Ndiyo njema uyashike haya: hatta tena yale usiyazuilie mkono; kwani amchaye Muungu atatoka katika haya yote.
- 19 Hekima nguvu zake mwenyi hekima
- 20 kuliko watu kumi watawalao mjini. Kweli, hapana mwana Adamu mwenyi haki duni-
- 21 ani afanyaye mema, asiyekosa. Tena usitie moyoni maneno yote yasemwayo; usije ukamsikia mtumwa wako akikutukana:
- 22 kwani marra nyingi tena moyo wako wajua kama wewe tena umewatukana wengine.
- 23 Haya yote nimethubutisha kwa hekima: nalisema, Nitakuwa na hekima, nayo ime-
- 24 farakana nami. Yaliyo mbali, na yaliyo
- 25 chini chini: yatatafutikana na nani. Nika-zunguka mimi, na moyo wangu wa kujua na kupeleleza, na kutafuta hekima, na shauri, na kuujua uovu ujinga, na kupiswa upu-
- 26 mpafu: nami nimeona wa uchungu kuliko mauti mwanamke mwenyi moyo wa mitego na shabuka, mikono ya mafungo: ampendezaye Muungu ataokoka kwake; lakini
- 27 mwenyi thambi atanaswa naye. Tazama,

haya niliyoyaona, asema Mhubiri, moja
 28 kwa moja, nilione shauri: inalolitafuta
 bado roho yangu, wala sikuliona; mwana-
 mume mmoja wa elfu nimemwona, mwana-
 29 mke kati yao wote sikumwona. Hili tu,
 tazama, nililoliona, kama Muungu amem-
 fanya mwana Adamu mwenyi adili; nao
 wametafuta mashauri mengi.

SURA 8.

N ANi kama mwenyi hekima? na nani
 ajuaye tafsiri la neno? Hekima ya
 mwana Adamu humng'ariza uso, na ugumu
 2 wa uso wake hubadiliwa. Mimi *nakupa*
shauri, Uishike amri ya mfalme, nayo kwa
 3 maana ya kiapo cha Muungu. Usiwe na
 haraka kutoka usoni pake, usisimame kwa
 neno baya: kwani afanya killa apendayo.
 4 Likiwa neno la mfalme mamlaka; na nani
 5 amwambiaye, Wafanyani? Ashikaye
 amri hatajua neno baya: na moyo wake
 mwenyi hekima hujua wakati na hukumu:
 6 kwani wa killa shauri uko wakati na hu-
 kumu; kwa kuwa mabaya ya mwana
 7 Adamu makubwa juu yake: kwani hajui
 yatakayokuwa; kwani nani atakayemweleza
 8 yatakuwaje? Hapana mwana Adamu
 mwenyi mamlaka juu ya roho aizuie roho;
 wala hana mamlaka juu ya siku ya kufa:
 walahapana kuachiliwa kwa vita: wala uovu
 9 hautamwokoia bwana wake. Haya yote
 nimeyaona, uikatia moyoni killa kazi iliyo-

- fanyika chini ya jua : wakati wa kuwa mwana Adamu mwenyi mamlaka juu ya
- 10 mwenziye kwa hasara yake. Nikaona pia waovu wamezikwa, nao wamefika *kaburini*; na katika mahali patakatifu wakaenda zao wakasahauliwa mjini waliofanya mema :
- 11 haya tena ubatili. Kwa kuwa hukumu juu ya kazi mbaya haitendeki upesi, kwa hiyo mioyo ya waana wa Adamu imejaa ndani
- 12 yao watende mabaya. Mwenyi thambi ajapofanya mabaya marra mia, na kuzidisha *siku* zake, lakini najua sana mimi itakuwa heri kwao wamchao Muungu, wachao mbele
- 13 yake: wala heri haitakuwa kwake mwovu, wala hatazidisha siku, zilizo kama kivuli :
- 14 akiwa haachi mbele ya Muungu. Kuna upumbafu uliofanyika juu ya inchi ; wawe wenyi haki wapatilizwao kama kwa kazi yao waovu ; tena wawe waovu wapatilizwao kama kwa kazi yao wenyi haki : nikasema,
- 15 Na haya pia ubatili. Ndipo nikasifu furaha mimi, kwa kuwa mwana Adamu hana lililo jema chini ya jua, kuliko kula, na kunywa, na kucheka : kwani ndiyo yatakayofuatana naye kwa kazi yake siku za maisha aliyo-mpa Muungu chini ya jua.
- 16 Nilipotia moyo wangu kujua hekima, na kuona utumwa uliofanyika juu ya inchi : (akiwa tena yuko asiyeona macho yake usi-
- 17 ngizi wala mchana wala usiku :) bassi nikaona kazi yote ya Muungu, ya kuwa haitafutikani na mwana Adamu kazi iliyofanyika chini ya jua : yakuwa, akisumbuka mwana

Adamu yo yote kuitafuta, haitafutikani :
hatta tena mwenyi hekima ajapothani ata-
ijua, hataweza lakini kuiona.

SURA 9.

- K**WANI haya yote nimeyatia moyoni,
hatta kuyatafutatafuta haya yote ;
ya kuwa wenyi haki, na wenyi hekima,
nazo huduma zao, mkononi mwa Muungu:
kama mapenzi kama machukio mwana
- 2 Adamu hajui : yote mbele yao. Yote sawa
sawa kwao wote : tukio moja kwake mwe-
nyi haki, na kwake mwovu : kwake aliye
mwema, aliye safi, na asiye safi : kwake
atoaye thabibu, na kwake asiyetoa : kama
mwema naye mwenyi thambi, aapaye kama
- 3 aogopaye kiapo. Ubaya huu katika yote
yaliyofanyika chini ya jua, ya kuwa wote
na tukio moja : hatta tena mioyo ya waana
Adamu imejaa ubaya, na upumbafu mio-
yoni mwao wakiwa hayi, hatta baadaye
- 4 huenda kwa wafu. Kwani kwake aamba-
tanaye na wahayi wote liko tumaini : kwani
mbwa hayi yeye heri kuliko simba aliyekufa.
- 5 Kwani wahayi hujua kama watakufa, laki-
ni wafu hawajui kitu, wala hawana tena
ijara ; kwani kumbukumbu lao limesahau-
- 6 liwa. Na mapenzi yao, na chukio yao, na
uwivu wao sasa umepotea ; wala hawana
tena sehemu milele kwa lo lote lililofanyika
chini ya jua.
- 7 Nenda zako kula kwa furaha chakula

- chako, ukanywe kwa moyo wa kicheko mvinyo yako, kwani Muungu amekwisha
- 8 kuzikubali kazi zako, Dayima mavazi yako yawe meupe; wala kitwa chako kisi-
- 9 kose marhamu. Uone maisha pamoja na mke umpendaye siku zote za maisha yako ya ubatili aliyokupa chini ya jua, siku zote za ubatili wako: kwani hii sehemu yako katika maisha na katika shughuli yako
- 10 uliyoshughulikia chini ya jua. Killa utakalopata mkono wako kufanya, fanya kwa nguvu zako; kwani hapana kazi wala shauri wala maarifa wala hekima kaburini uendako.
- 11 Nikarudi nikaona chini ya jua, kama si ya wapesi mashindano, wala si ya mashujaa vita, wala si ya wenyi hekima chakula, wala tena si ya wenyi akili utajiri, wala tena si ya wenyi maarifa upendeleo; lakini
- 12 wakati na ajali huwapata wote. Kwani na mwana Adamu hajui wakati wake; kama samaki zilizokamatwa na wavu mbaya, na kama ndege zilizonaswa na shabuka, vivyo waana Adamu hutegwa na wakati mbaya, ukiwaangukia ghafula.
- 13 Hivyo tena nimeona hekima chini ya jua,
- 14 nayo mkuu kwangu: kulikuwa na mji mdogo, na watu ndani yake haba; akaja juu yake mfalme mkubwa, akauzunguka,
- 15 akaujengea maboma makubwa: basi akatokea humo mtu maskini mwenyi hekima, naye akauokoa mji ule kwa hekima yake; wala mwana Adamu ye yote hakumkumbuka

18 KOHELETH ao MHUBIRI, 9.

- 16 yule mtu maskini. Nikasema mimi, Heri hekima kuliko ushujaa: illakini hekima yake maskini yatharauliwa, maneno yake hayasikiwi.
- 17 Maneno yake mwenyi hekima kwenyi utulivu husikiwa kuliko kilio chake atawa-
- 18 laye kati ya wapumbafu. Heri hekima kuliko selaha ya vita: lakini mwenyi thambi mmoja huyaharibu mema mengi.

SURA 10.

- M**AINZI mafu hukokomoza uvundo marhamu yake mfanyi manukato: upumbafu haba hupita kwa uzito hekima
- 2 na heshima. Moyo wake mwenyi hekima kwa kuume: lakini moyo wake mpumbafu
- 3 kwa kushoto. Hatta tena mpumbafu aendapo njiani, hupungukiwa, naye humwambia killa mtu, ndiye mpumbafu.
- 4 Icho yake atawalaye ikipanda juu yako, usiache mahali pako; kwani upole hutuliza
- 5 thambi zilizo kuu. Uko ubaya niliouona chini ya jua, utokao kama kwa kupitiwa
- 6 mbele yake mwenyi mamlaka: upumbafu huwekwa pa juu sana, nao wakwasi hukaa chini. Nimeona watumwa wamepanda frasi, na wakuu wakitembea kama watumwa
- 8 katika inchi. Achimbaye shimo atalitumbukia: naye abomaye kitalu nyoka atamwuma. Avunjaye mawe ataumizwa nayo;
- 10 achanjaye miti, huona hatari nayo. Kama chuma hakipati, mtu asipoinoa ncha hana

buddi kutia nguvu zayidi : lakini hekima
 11 yafaa kufanikisha. Nyoka akiuma kabla
 ya kutumbuika, bassi haina fayida yake mtu-
 12 mbuizi. Maneno ya kinwa chake mwenyi
 hekima neema : midomo yake mpumbafu
 13 itammeza mwenyewe. Mwanzo wa maneno
 ya kinwa chake ujinga : na mwisho wa
 14 masemo yake upumbafu mbaya. Mpumbafu
 tena huongeza maneno : mwana Adamu
 hajui yatakayokuwa, nayo yatakayokuwa
 15 baada yake nani atakayemweleza? Kazi
 yao wapumbafu huwachosha wote, kwani
 16 hajui auendeeje mji. Ole wako, inchi,
 akiwa ufalme wako kijana, nao wakuu
 17 wako hula assubuhi! Heri nawe, Ee inchi,
 mfalme wako akiwa mwana wa wakuu, na
 masheki hula wakati wake, wapate nguvu,
 18 wala si ulevi! Kwa uvivu dari hutu-
 mbukia, na kwa mikono ya utepetevu
 19 nyumba huvuja. Kwa kicheko hufanyizia
 chakula, na mvinyo hufurahisha maisha :
 20 nayo fetha ijibiayo vyote. Mfalme msimtu-
 kane, wala si niani mwako ; wala usiwatu-
 kane wakwasi katika chumba chako cha
 kulala : kwani ndege ya anga ataichukua
 sauti, na mwenyi mabawa atalitangaza neno.

SURA 11.

TUPA chakula chako usoni pa maji :
 2 kwani utakiona baada ya siku nyingi.
 Uwagawie saba na hatta wanane sehemu ;
 kwani hujui ubaya gani utakaokuwa juu

- 3 ya inchi. Mawingu yakijaa maji yajimi-
 mina juu ya inchi: na mti ukianguka
 kusini, ao kaskazini, mahali uangukapo
 4 mti, ndipo utakapokuwapo. Aangaliaye
 upepo hatapanda; atazamaye mawingu
 5 hatavuna. Ukiwa hujui njia ya upepo,
 ginsi ya mifupa ya mtoto katika mimba
 yake aliye mzito; vivyo hujui matendo ya
 6 Muungu atendaye vyote. Assubuhi panda
 mbegu zako, wala jioni usiuzuie mkono,
 kwani hujui yatakayofanikiwa, kama haya
 7 kama yale, ao kama yote sawa mema. Kweli
 nuru tamu, nalo jema machoni kutazama
 8 jua. Hatta akiishi mwana Adamu miaka
 mingi, aifurahie yote: naye azikumbuke
 siku za giza, kwani zitakuwa nyingi. Yote
 yajayo ubatili.
- 9 Ufurahie, Ee kijana, utoto wako; na
 moyo wako ukufurahishe siku za ujana
 wako, ukaziendee njia za moyo wako, na
 kwa kuona kwa macho yako: lakini ujue,
 kwa haya yote Muungu atakuletea hukumu.
- 10 Bassi ufarakishe huzuni moyoni, ukaondoe
 ubaya mwilini: kwani utoto na wakati wa
 kiume ubatili.

SURA 12.

UMKUMBUKE Muumba wako siku
 za ujana, kabla hazijaja siku zilizo
 mbaya, wala kukaribia miaka, utakapose-
 2 ma, Sina furaha nayo; kabla jua, na nuru,
 na mwezi, na nyota hazijatiwa giza, wala

- kuregea mawingu baada ya mvua: siku watakayotetemeka walinzi wa nyumba, nao
- 3 kujiinama wenyi nguvu, nao wasagaji wakikoma kwa kuwa haba, nao watazamao
- 4 madirishani kutiwa giza, na milango kufungwa njiani; kitakaposhushwa kishindo cha kusagia, na mtu huondoka kwa sauti ya ndege, na binti zote za uimbo watainamishwa; hatta wataogopa yaliyo juu na njiani hofu; nao mlozi utachanua maua, naye panzi atalemea, nayo pilipili itakosa: kwa sababu aenda mwana Adamu kwa nyumba yake ya milele, nao waombolezao
- 6 huzuguka njiani: kabla haijafunguka kamba ya fetha, ao bakuli ya thahabu kuvunjika, ao mtungi kupondwa kisimani, ao gurudumo kuvunjika birikani; nayo mavumbi kurudi katika inchi kama yalivyo kuwa, na roho kumrudia Muungu aliyeitoa.
- 8 Ubatili wa ubatili, asema Mhubiri; yote ubatili.
- 9 Na tena, kwa kuwa Mhubiri mwenyi hekima akazidi kuwafundisha watu maarifa; hatta akafikiri, akatafutatafuta, akatengeneza methali nyingi. Mhubiri akataka kupata maneno ya kukubalika, na maandiko ya adili, maneno ya kweli.
- 11 Maneno yao wenyi hekima kama michokoo, na kama mismari iliyotiwa sana maneno ya mabwana wa makusanyiko huto-
- 12 lewa na mchungaji mmoja. Hatta zayidi ya haya, mwanangu, uonywe: wa kufanyiza

vitabu vingi hapana mwisho; na kusoma sana kwa chokesha mwili.

- 13 Mwisho wa neno; yote yamesikiwa :
Muungu umche, ukazishike amri zake ;
- 14 kwani ya mwana Adamu yote haya: Kwani
Muungu ataleta killa kazi hukumuni, kwa
killa jambo la siri, likiwa jema ao likiwa
baya.

UIMBO WA NYIMBO.

SO
LI
DEO
GL
OR
IA

ZANZIBAR:

PRINTED AT THE UNIVERSITIES' MISSION PRESS.

1888.

UIMBO WA NYIMBO.

UIMBO wa nyimbo, ulio wa Sulemani.

- 2 Anibusu kwa busu za kinwa chake;
Kwani heri mapenzi yako kuliko mvinyo.
- 3 Manukato yako yanukia vizuri;
Manukato yaliyomiminika jina lako;
Kwa hiyo waanawali hukupenda.
- 4 Univute; nyuma yako tutakimbia;
Mfalme amenileta vumbani kwake:
Tutafurahi, tutakushangilia,
Tutayanena mapenzi yako kuliko mvinyo:
Kwa adili hukupenda.
- 5 Mweusi mimi, mzuri lakini,
Enyi binti Yerusalemi,
Kama hema za Kedar,
Kama mapazia ya Sulemani.
- 6 Msinitazame kwa kuwa mwekundu,
Kwa kuwa jua limenichungulia.
Wana wa mamanga walikuwa wamekasi-
rika nami,
Wameuiweka nilinde mizabibu;
Wala mizabibu yangu mimi sikuitunza.
- 7 Unielezee, ewe nikupendaye rohoni,
Wapi ulishapo *kundi*, wapi uwalazapo
aththuuri:
Kwani mbona niwe kama aliyefunikwa
Karibu na makundi ya wenzako?

- 8 Usipojua mwenyewe, uliye mzuri kati ya
 waanawake,
 Nenda zako kufuata nyayo za kondoo,
 Ukawalishe waana mbuzi wako kaudo la
 hema za wachungaji.
- 9 Nimeki linganisha, Ee mpendwa wangu,
 Na frasi wa magari ya Farao.
- 10 Machavu yako mazuri na mistari,
 Shingo lako na mikufu.
- 11 Tutaku'anyia mistari ya thahabu
 Yenji vipini vya fetha.
- 12 Akiwapo mezani pake mfalme,
 Nardo yangu ikatoa harufu yake.
- 13 Mfuko wa manemaume kwangu mpenzi
 wangu,
 Ukaao kati ya maziwa yangu.
- 14 Chana cha hina kwangu mpenzi wangu,
 Mizabibuni kwa Engedi.
- 15 Tazama, mzuri wewe, mpenzi wangu:
 tazama, wewe mzuri;
 Njiwa macho yako.
- 16 Tazama, mzuri wewe, mpenzi wangu, tena
 mtamu;
 Nacho kitanda chetu chanikiwit.
- 17 Mierezi boriti za nyumba yetu,
 Miti yetu miberoshi.

SURA 2.

MIMI waridi wa Sharon,
 Nyinyoro ya boondeni.

- 2 Kama nyinyoro kati ya miiba,
Mpendwa wangu vile kati ya binti.
- 3 Kama mtofaa kati ya miti ya msitu,
Mpenzi wangu vile kati ya waana.
Nikipendezwa nimekaa chini yake kivulini,
Na matunda yake matamu kwa kuaka
lengu.
- 4 Akanileta hatta nyumba ya karamu,
Na bandera yake juu yangu mapenzi.
- 5 Nitegemezeni na vichala vya mzabibu,
niburudisheni na tofaa:
Kwani mapenzi yameuishika mimi.
- 6 Mkono wake wa kushoto chini ya kitwa
changu,
Na mkono wake wa kuume wanikumbatia.
- 7 Nawaapiza ninyi, binti Yerusalemi,
Kwa paa na kwa ayyala za mwitu,
Msiondokeshe, msiamshe mapenzi,
Hatta yatakapoona vema.
- 8 Sauti ya mpenzi wangu! Tazama, anakuja,
Akiruka mihuni, akirukaruka vilimani.
- 9 Mpenzi wangu afanana na paa, ao mwana
ayyala:
Tazama, asimama nyuma ya ukuta wetu,
Achungulia madirishani,
Ajionyesha kwenyi vipande.
- 10 Mpenzi wangu akanena, akaniambia,
Ondoka, mpendwa wangu, mzuri wangu,
uje zako.
- 11 Kwani, tazama, baridi imepita,
Musika imekwisha imekwenda zako;

- 12 Maua yatokea katika inchi;
Wakati wa kuinba umewadia,
Na sauti ya hua husikiwa katika inchi yetu;
- 13 Mtini hupevusha tini zake changa,
Mizabibu huchanua,
Hutoa harufu nzuri.
Ondoka, mpendwa wangu, mzuri wangu,
uje zako.
- 14 Ee njiwa wangu, wa mapangoni kwa jabali,
wa mafichoni penyi palipochongoka,
Nitazame uso wako, nisikie sauti yako;
Kwani tamu sauti yako, na uso wako mzuri.
- 15 Ututwalie mbweha, mbweha wadogo, wa-
haribuo mizabibu;
Kwani mizabibu yetu inachanua.
- 16 Wangu mimi mpenzi wangu, nami wake:
Hulisha kati ya nyinyoro.
- 17 Hatta mchana uvumapo matlai, na vivuli
kukimbia mbali.
Geuka, mpenzi wangu, uwe kama paa ya
mwana ayyala juu ya milima ya Bether.

SURA 3.

- U**SIKU kitandani nalimtafuta roho
yangu impendaye:
Nalimtafuta nisimpate.
- 2 Haya nitondoka nitazunguka mji,
Njiani na mitaani,
Nitamtafuta roho yangu impendaye,
Nalimtafuta nisimpate.
- 3 Wakampata walinzi wazungukao mjini:

Nikawaambia, Yeye, roho yangu impendaye,
ye, umemwona?

- 4 Punde nikawapita tu,
Nilipompata roho yangu impendaye:
Nikamshika, nisimwache,
Hatta nilipomleta nyumbani kwa mama-
ngu,
Chumbani kwake aliyenizaa.
- 5 Nawaapiza ninyi, binti Yerusalemi,
Kwa paa na kwa avyala za mwitu,
Msiondokeshe, msiamshe mapenzi,
Hatta yatakapoona vema.
- 6 Nani huvu apandaye katika jangwa kama
nguzo za moshi,
Ametiwa manukato ya mauemane na uvu-
mba,
Kwa marashi yote ya mchuruzi?
- 7 Tazama, machela ya Sulemani ndiyo:
Mashujaa settini wazungukao,
Wa mashujaa wa Israeli.
- 8 Wote washikao upanga, wamehitimu vitani:
Killa mtu na upanga wake pajani mwake,
Kwa hofu za usiku.
- 9 Mfalme Sulemani alijifanyizia gari
La miti ya Lebanoni.
- 10 Akafanviza nguzo zake fetha,
Chini yake thahabu, kikao chake urujuani,
Kati yake ujumu ya mapenzi
Ya binti Yerusalemi.
- 11 Tokeni, enyi binti Sayuni, mtazameni
mfalme Sulemani,
Mwenyi taji aliyomvika mamaye siku ya

maposo yake,
Siku ya furaha ya moyowe.

SURA 4.

- T**AZAMA, wewe mzuri, mpendwa wa-
ngu; tazama, mzuri wewe;
Macho yako njiwa nyuma ya barakoa yako;
Nyele zako kama kundi la mbuzi,
Walalao upande wa mlima Gilead.
- 2 Meno yako kama kundi lao waliokatiwa
suffuf,
Wapandao katika kuoshwa;
Wote wenyi mapacha,
Wala hapana aliyefiwa miongoni mwao.
- 3 Midemo yako kama kamba nyekundu,
Na zuri kanwa lako:
Paji la uso wako kama kipande cha kamma-
manga
Nyuma ya barakoa yako.
- 4 Shingo lako kama mnara wa Daud, ulio-
jengwa pakuwekea selaha,
Vilimotundikwa vigao elfu,
Ngao zote za mashujaa.
- 5 Maziwa yako mawili kama mapacha mawili
wachanga wa paa,
Walishwao kati ya nyinyoro.
- 6 Hatta mchana uvunapo matlai, na vivuli
kukimbia mbali,
Nitakwenda zangu hatta mlima wa man-
mane.

- Hatta kilima cha uvumba.
- 7 Mzuri pia wewe, mpendwa wangu;
Wala kwako hapana nawaa.
- 8 Pamoja nami katika Lebanoni, bibi harusisi,
Pamoja nami katika Lebanoni, njoo:
Tazama katika kilele cha Amana
Katika kilele cha Senir, ua Hermon,
Katika mapanga ya simba,
Katika milima ya chui.
- 9 Umenitia moyo, umbu langu, bibi harusisi;
Umenitia moyo kwa jicho lako moja,
Kwa mkufu mmoja wa shingo lako.
- 10 Mapenzi yako ginzi yalivyo mazuri, umbu
langu, bibi harusisi!
Ginzi yalivyo heri mapenzi yako kuliko
mvinyo!
Na harufu za marhamu zako kuliko manu-
kato ya namna zote!
- 11 Midomo yako, bibi harusisi, yatiririka ya
asali,
Asali na maziwa chini ya ulimi wako;
Na harufu ya mavazi yako kama harufu ya
Lebanoni.
- 12 Bustani iliyofungwa umbu langu, bibi
harusisi;
Kisima kilichofungwa, chemchemi iliyoti-
wa muhuri.
- 13 Machupuzi yako shamba la mikamma-
manga, lenyi matunda ya thamani;
Mihina ua minardo,
- 14 Nardo na zafarani,
Kane na mdalasini, na miti yote ya uvumba;

UIMBO WA NYIMBO 4.

Manemane na uudi, na manukato yote
ya'liyo makuu.

15 Chemchemi ya bustani *wewe*,

Kisima cha maji mazima,

Na mito itokayo Lebanoni.

16 Amka, Ee kaskazi; njoo, kusi;

Vuma juu ya bustani yangu, yatokee
manukato yake.

Aje mpenzi wangu bustanini mwake,

Akale matunda yake ya thamani.

SURA 5.

NIMEK UJA bustanini mwangu, umbu
langu, bibi harusisi:

Nimechuma manemane yangu pamoja na
manukato yangu;

Nimekula kamba la asali pamoja na asali
yangu;

Nimekunywa mvinyo yangu pamoja na ma-
ziwa yangu.

Kaleni, enyi rafiki;

Nyweni, hatta nywemi sana, enyi wapenzi.

2 Nalikuwa nimelala mimi, moyo wangu uka-
wa macho:

Sauti ya mpenzi wangu abishaye,

Unifungulie, umbu langu, mpendwa wa-
ngu, njiwa wangu, mkamilifu wangu;

Kwani kitwa changu kimetiwa umande
sana,

Nyole zangu manyunyo ya usiku.

3 Nimevua kaulu yangu; nipateje kuivaa?

- Nimetawaza migun: nipateje kutia tuka?
- 4 Mpenzi wangu akauingiza ukono wake
tunduni,
Moyo wangu ukachafuka kwa ajili yake.
- 5 Naliondoka, nimfungulia mpenzi wangu;
Mikono yangu ikatiririka manemane,
Vidole vyangu manemane yenyi kudondo-
ka;
- Juu ya vipimi vya kemeo.
- 6 Nikamfungulia mimi mpenzi wangu;
Naye mpenzi wangu akawa ametoweka,
amekwenda zake.
Roho yangu imetoka, alipokisema:
Nilimtafuta nisimpate;
Nalimwita asinijibu.
- 7 Wakanipata walinzi wazungukao mjini.
Wakanipiga, wakanijeruhi;
Walinzi maboma wakaninyanganya shela.
- 8 Nawaapiza ninyi, hinti Yerusalemi, mki-
mwona mpenzi wangu,
Mwambie, kama nimi yamenishika mape-
nzi.
- 9 Mpenzi wako nani kuliko mpenzi *mwingine*,
Wewe uliye mzuri, miongoni mwa walina-
wake?
Mpenzi wako nani kuliko mpenzi *mwingine*,
Utwapize hivi?
- 10 Mpenzi wangu mweupe na mwekundu,
Miangulifu wa elfu kumi.
- 11 Kitwa chake thababu safi tenle,
Nyele zake za singa nyingi, nyensi kama
kunguru.

- 12 Macho yake kama njiwa mitoni pa maji;
Walioosha na maziwa, yamewekwa kwa
utimilifu.
- 13 Machafu yake kama tuta la manukato,
minara ya marhamu:
Midomo yake nyinyoro zitiririkazo mane-
mane yenyi kudondoka.
- 14 Mikono yake pete za thahabu zilizotiwa
zabarajadi.
Kiwiliwili chake kazi ya pembe iliyofuni-
kizwa na yakuti samawati.
- 15 Miguu yake nguzo za maburi zilizotege-
mea maweko ya thahabu safi:
Sura yake kama Lebanoni, teule kama
mierezi.
- 16 Kanwa lake lililo tamu: hakika yu mzuri
pia.
Huyu mpenzi wangu, huyu rafiki yangu,
Enyi binti Yerusalemi.

SURA 6.

A MEKWENDA wapi mpenzi wako,
Wewe uliye mzuri kati ya waana-
wake?

Ameguka wapi mpenzi wako,
Tumtafute pamoja nawe?

- 2 Mpenzi wangu ameshuka kwa bustani
yake, kwa matuta ya manukato,
Kulisha bustanini, kuchuma nyinyoro.
- 3 Mmi wake mpeuzi, na wangu mimi mpenzi:
Aishaati ya nyinyoro.

- 4 Mzuri wewe, mpendwa wangu, kama Tirza,
Mwenyi neema kama Yerusalemi,
Wa kuogofya kama wenyi bandera.
- 5 Unigeuzie mbali macho yako,
Kwani yamenishinda.
Nyele zako kama kundi la mbuzi,
Walalao upande wa Gilead.
- 6 Meno yako kama kundi la kondoo,
Wapandao katika kuoshwa;
Wote wenyi mapacha,
Wala hapana aliyefiwa miononi mwao.
- 7 Paji la uso wako kama kipande cha kamma-
manga
Nyuma ya barakoa yako.
- 8 Wako malkia settini, na masuria themanini,
Na waanawali wasio na hesabu.
- 9 Njiwa wangu, mkamilifu wangu, mmoja
yeye;
Wa pekee yeye wa mamaye;
Yeye mteule wake aliyemzaa.
Wakimwona binti humwita heri:
Malkia wao, na masuria, humsifu.
- 10 Nani huyu atazamaye kama mapambazuko,
Mzuri kama mwezi,
Safi kama jua,
Wa kuogofya kama wenyi bandera?
- 11 Nalishuka hatta bustani ya mijozi,
Kuyona machipuko ya boondeni,
Kuona kama mzabibu umechanua,
Kama mikammananga imetoa maua.
- 12 Ndipo nami, nisipojua, roho yangu ikani-
waka

Magari ya watu wangu wakarimu.

- 13 Rudi, rudi, Ee Mshulammi;
Rudi, rudi, tukutazame.
Mtairtazamiani Mshulammi,
Kama mchezo wa Mahanaim?

SURA 7.

- G**INSI ilivyo mizuri miguu yako na
viatu, Ee bin i mkarimu!
Vifundo vya mapaja yako kama johari,
Kazi ya mikono ya mtu mstadi.
- 2 Kitofu chako bakuli la uviringo,
Lisilokosa mvinyo iliyochanganyika:
Tumbo lako chungu ya ngono,
Iliyofungiwa nyinyoro.
- 3 Maziwa yako mawili kama mapacha mawili
Nao wachanga wa paa.
- 4 Shingo yako kama mnara wa pembe;
Macho yako maziwa ya Heshbon, mlangoni
pa Bath-rabbim;
Pua yako kama mnara wa Lebanoni
Utazamao Dameski.
- 5 Kitwa chako juu yako kama Karmel,
Na nyele za kitwa chako kama pofuro;
Mfalme hufungwa katika mistari yake.
- 6 Ginsi yalivyo mazuri, ginsi yalivyo mata-
mu,
Mapenzi, kwa hanassa!
- 7 Urefu wako huu umefanana na mnazi,
Maziwa yako na vichala vya mzabibu.
- 8 Nalisema, Nitapanda mnazini,
Nitayashika makuti yake;

- Maziwa yako yawe kama vichala vya mza-
 bibu,
 Na harufu ya pumuzi yako kama tofaa ;
 9 Na kinwa chako kama mvinyo iliyo bora,
 Imezwayo marithawa na mpenzi wangu,
 Ikitiririka midomoni mwao walalao.
- 10 Mimi wake mpenzi wangu,
 Na tamaa yake kwangu mimi.
- 11 Njoo, mpenzi wangu, tutoke twende ma-
 shambani ;
 Tukalale katika vijiji.
- 12 Tuankie mizabibuni ;
 Tuone kama mزابibu umechanua, macha-
 nga yake yamefunuka,
 Mikamamanga ikitoa maua :
 Ndipo nitakupa mpenzi yangu.
- 13 Lufafi hutoa harufu,
 Na milangoni mwetu namna zote za yenyi
 thamani, mapya na ya kale,
 Ni iyokuwekea, Ee mpenzi wangu.

SURA 8.

- L**AITI ungekuwa kama ndugu yangu,
 Aliyenyonya maziwa ya mamangu!
 Nikikuona nje, ningekubusu ;
 Tena, asinitharau mtu.
- 2 Ningekuongoza kukuleta nyumbani kwa
 mamangu,
 Naye angenifundisha ;
 Ningekunywesha mvinyo iliyokolea,
 Maji ya kamamanga yangu.

3 Mkono wake wa kushoto chini ya kitwa
changu,
Na mkono wake wa kuume ungenikumba-
tia.

4 Nawaapiza ninyi, binti Yerusalemi,
Msion-lokeshe, msiamshe, mapeuzi,
Hatta yatakapoona vema.

5 Nani huyu apandaye katika jaagwa,
Akimtegemea mpenzi wake?

Chini yake mtofaa nalikuamsha :
Ndipo alipokuonea utungu mainako,
Ndipo alipoona utungu aliyekuzaa.

6 Unitie kama muhuri moyoni mwako,
kama muhuri mkononi mwako :

Kwani mwenyi nguvu kama mautili upendo;
Mgumu kama ahera uwivu :
Kuwaka kwake kuwaka kwa moto,
Ndimi za moto za Yah.

7 Maji mengi hayawezi kuuzimia upendo,
Wala gharika kuufurika :

Angetoa mtu mali yote ya nyumbaye badala
ya upendo,
Kutharauliwa angetharauliwa.

8 Kwetu umbu mdogo,

Wala maziwa hana :

Tumfanyieje umbu letu.

Siku atakapofanyiwa maneno?

9 Akiwa ukuta tutamjengea menomeno ya
fetha :

Naye akiwa mlango,

Tutamfunikia mbau za erezi.

- 10 Mimi ukuta, na maziwa yangu kama minara:
 Ndipo nilipokuwa.
 aliyeona salama.
- 11 Sulemani alikuwa nayo mizabibu kwa Baalhamon,
 Akawapangisha mizabibu waliuzi;
 Killa mtu alete ya matunda yake elfu za fetha.
- 12 Mizabibu ya kwangu, iliyo yangu, mbele yangu:
 Kwako Ee Sulemani, elfu,
 Na miteen kwao walinda matunda yake.
- 13 Wewe ukaaye bustanini,
 Wenzako hukusikilizia sauti:
 Unisikize mimi.
- 14 Ufanye haraka, mpenzi wangu,
 Uwe kama paa, au kama mwana ayyala
 Juu ya milima ya manukato.

MWISHO.

